# Ziara Ya Mhariri Nchini Uganda: Alivyovutiwa Na Shule



*MHARIRI wetu,* **Bw. Abdulrahman Sheriff** *alikuwako nchini Uganda kwa ajili ya shughuli za kazi na kampuni yake ya SGS KENYA LTD na katika ziara hiyo. Katika ziara yake ya Uganda Kaskazini wilayani Lira, alitembelea shule ya Sekondari ya Ngai na alivutiwa sana na maendeleo ya shule hiyo na hapa antusimulia.....*

**KATIKA ziara hiyo ambayo nilifuatana na wafanyakazi wa Coffee Marketing Board Bw. Caesar Olwor, Bw. Jonathan Egach Kabaka, Bw. Uringi Okello; Bw. Lazaro Biryabarema na Bw. Jimmy Segawa Katumba- tulivutiwa sana na hatua kubwa iliyofanywa na shule hiyo katika kujitegemea kwa mambo mengi.**

**Tulikutana na Mwalimu Mkuu wa shule, Bw. Charles Opio Akome ambaye alitueleza kwa kirefu vile shule hiyo inavyojitegemea yenyewe na jinsi wanafunzi wanavyopata matunda kwa jasho lao wenyewe.**

**Bw. Akome alinifahamisha kwamba shule hiyo ya Ngai ilianzishwa mwaka 1981 na kwa miaka miwili pekee imeweza kupiga hatua ya kujitegemea hasa wanafunzi wenyewe ambao hujitolea kulima na kujipatia manufaa baada ya kuvuna mavuno yao.**

## *NJUGU*

**Shule hiyo ina shamba kubwa la tumbaku, wanalima mahindi, njugu, maharagwe, na sasa wako katika mpango wa kulima serena, mtama na sunflower. Mavuno wanayoyapata wanafunzi hao yanauzwa na kuwafaidia mambo mengi.**

**Mwalimu Mkuu, Bw. Akome alisema kwamba wanafunzi hawalazimishwi kulima bali wale wanalima hufaidika kwani mazao yanapouzwa, hujilipia karo, hupewa mavazi ya shule bure na pia chakula cha mchana hupikiwa hapo hapo.**

## *VIPINDI*

**Alipoulizwa kama kuna vipindi maalum vya ukulima kwa wanafunzi, Bw. Akome alisema hakuna vipindi hivyo na wanafunzi wanalima wakati wao wa kupumzika. "Kila mwanafunzi anapewa laini moja pekee na akipata nusu saa ya mchana ama jioni kabla ya kwenda nyumbani ndipo anajifanyia kazi yake kwa hivyo hakuna wakati wowote ambao wanafunzi wanaupoteza kwa ajili ya ukulima", akaongeza Mwalimu huyo Mkuu.**

**Pato kubwa linalopatikana kaitka shule hiyo linatokana na tumbaku ya sigara. Kuna shamba kubwa kuliko ya mazao mengine na kuna stoo ambazo zimejengwa maalum kwa ajili ya ukaushaji tumbaku hiyo na pia chumba kimoja cha kuwekea mazao ambayo tayari kwa kuuzwa.**

**Hakika mipango ya shule hiyo yalinivutia na kutoa shauri kwa waalimu wakuu hasa wa shule za vijijini watafanikiwa sana ikiwa watafanya mipango hii. Kwani wale wazazi ambao hawana uwezo wa kulipa karo huondokewa na taabu hiyo ikiwa wanafunzi watajitegemea wenyewe.**

**Mipango ya shule hiyo ya Ngai inastahili kuanzishwa hapa nchini kwani kwanza huwafanya wanafunzi kujifundisha kulima na baada ya masomo ikiwa atakosa kazi, atakuwa tayari kwenda shambani na kulima. Pili, hujitegemea kwa mavazi pamoja na chakula cha mchana kwa yale mazao wanayolima**

**Sehemu nyingine za kuvutia nilizotembelea ni pamoja kwenye chemchemi za Maji ya Moto "Hot Spring" huko Bundibugy. Katika sehemu hiyo, ndipo kuna milima mikubwa sana na hata ukiwako katika gari utakuta chini yafika maili moja ama mbili Maji ya kwenya milima hiyo huwa meupe sana na ladha ya kupendeza.**



*BW. AKOME*

**Miji mingine ambayo tuliyotembelea ni pamoja na Masaka, Mbarara, Lira, Fort Portal, Hoima, Gulu, Pakwach, Nebbi, Tororo, Soroti, Mbalc, Mbale na mji mkuu wa Kampala. Ziara hiyo ilikuwa ya kazi na muda tuliotumia ni karibu mwezi mzima.**



*Wanafunzi wa Ngai wanajishughulisha kuchambua Tumbaku na kuweka kwa gredi tafauti.*

# Asemavyo Mhariri:



• A. S. MWIDANI



• SAMUEL NDORO

## Pongezi Meya Na Mdogo Wako

NACHUKUA fursa hii kumpongeza **Diwani Ahmed Shahame Mwidani** kwa kuchaguliwa kuwa Meya Mpya wa Jiji la Mombasa na pia pongezi kwa **Diwani Samuel Ndoro** kupewa mamlaka ya Naibu wa Meya. Na Pia nawapongeza Madiwani wote waliopewa jukumu la kuongoza idara tafauti katika Baraza la Mji; kazi ambazo ni za kuwatumikia wananchi wote na kuleta sura mpya ya usafi wa mji na mambo mengine muhimu ambayo hayakuwahi kutekelezwa hapo awali.

KUCHAGULIWA kwa Diwani Mwidani kama Meya wa Mombasa halikuwa jambo la kushangaza kwani ni diwani wa pekee kati ya madiwani waliochaguliwa kwa kura, kupitishwa na watu wa sehemu yake ya Port Reitz bila ya kupingwa; dalili ambayo ilikuwa wazi juu ya kazi aliyowafanyia wananchi wa sehemu yake ambao bila ya tashwishi waliamua kwa kauli moja kumchagua na kumpitisha mapema kuliko madiwani wengine ambao walibidiika wapate upinzani.

HAKUNA wasiwasi Diwani Mwidani atakitumikia cheo hicho cha Umeya kwa uhodari wa ujuzi alionao katika Manispaa hiyo kwani ni mmoja ambaye amekuwa diwani wa siku nyingi katika wale walioko ndani ya Manispaa hiyo na pia katika Baraza lilopita, alikuwa kama Meya Mdogo; cheo ambacho alikitumikia kwa uwezo wake wa uongozi na kazi yake ilisifiwa sana sio na madiwani wenzake pekeee walioamua kumpa madaraka mapya bali hata wananchi wote wa Mombasa.

JAMBO la kufurahisha zaidi kwa Diwani Mwidani alilolifanya mara baada ya kuteuliwa kama Meya ni kufuatana na madiwani wenzake na kutemebelea afisi ya Kanu na kutoa shukrani kwa chama. Diwani Mwidani alisema Kanu ndicho kilichotoa kibali kwa viongozi kusimamia kura na kwa hivyo viogozi wanabidiika kukiheshimu chama na akaahidi kuwa Manispaa ya Mombasa itashirikiana kila wakati na Kanu katika kuleta maendeleo ya Mji.

IKIWA viongozi wote waliochaguliwa kutoka Wauunge, Madiwani watashirikiana na Kanu, basi nina uhakika makubwa yatapatikana katika mji huu. Viongozi wote wanawajibika na wanastahili kushirikiana kikamilifu na chama kwani Kanu ndio iliyowafanya leo hii wakaitwa viongozi; bila ya Kanu hawangekuwa viongozi.

UMEFIKA wakati viongozi wa Mombasa na Pwani nzima kuwa kitu kimoja na kutimiza wajibu wa ahadi walizotoa wakati wa kupigania viti- wananchi wa Pwani wamechoka na migogoro ya viongozi wao na wanachotaka ni viogozi wote kushirikiana katika kupiga hatua kubwa ya maendeleo na hakuna lisowezekana ikiwa viongozi watakuwa kitu kimoja, basi wananchi watapata manufaa na maendeleo ya kudumu ya mkoa wetu wa Pwani

**- Abdulrahman Sheriff.**



## Amir Ashinda Funzi

*DIWANI mpya wa kisiwa cha Funzi katika Kwale Kusini, Bw. Mohammed M. Amir ametoa shukrani nyingi kwa wananchi wa sehemu hiyo kwa kumteua yeye kama diwani wa sehemu hiyo.*


*Bw. Amir aliahidi kuwatumikia ipasavyo katika harakati ya kuinua na kuleta maendeleo ya sehemu hiyo. Pia aliwashukuru wakuu wa tawala na maafisa wote waliosimamia uchaguzi huo bila ya mapendeleo.*

*Aliahidi kutimiza ahadi alizotoa wakati wa kampeni na akasema atashirikiana na viongozi wenzake katika kuleta maendeleo ya kudumu katika Kwale Kusini.*

# Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI
VYA FARUCCI KWA MSHINDI
WA KWANZA NA T-SHIRT
KWA WASHINDI WA PILI
NA WATATU KATIKA SHINDANO
JIPYA LA KUJAZA MANENO

## SWAHILI CROSSWORD No. 173



*KWENDA KULIA:*

1. Sumu ya nyoka au ya mshale.
5. Silaha ya kuwindia ndege.
6. Tenzwa nguvu.
7. Moja katika makontinenti ya dunia.
9. Jina la kibaniani
12. Ndani kwa kimombo.
13. majani ya mnazi
14. Medical Officer
15. Sana
16. Chombo kama bangili.
17. Namna ya kukaa
18. Jitu zima.

*KWEND CHINI:*

1. Mti unaosaidia chombo kukipeleka maji mengi.
2. Kiungo cha mchuzi.
3. Sehemu ya juu ya kichwa.
4. Duara, Mvingo, ua.
8. Kinyume cha iuze
10. Aina ya mti.
11. Sikiza mwito.
14. Karne moja.
16. Ufupi wa "kazana kusoma".

**Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 172.**

1. S. A. Msaada, Sanduku La Posta 98106, MOMBASA.
2. Islam Ali Swedan, Sanduku La Posta 62, MARIAKANI.
3. Miss Madango Essau, Sanduku La Posta 85390, MOMBASA.

*Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANANO No. 172.**

*KWENA KULIA*

1. BAWABU, 5. JUA, 6. RAFIKI, 8. MA, 10. KIRIBA, 12. KAMATANA, 15. UN, 16. MKIZI, 18. AKUTOE, 19. SI.

*KWENDA CHINI*

1. BARAKA, 2. ALIKA, 3. UJIRA, 4. KAMBA, 7. KITAMBO, 9. AA, 11. INDIA, 13. MUNYU, 14. BISI, 17. UA.

**JINA.......................................**

**SANDUKU LA POSTA..........................**

............................................

**Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwe Muhariri *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **Nov. 9. 1983.** saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.